

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULIZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO

09 JUNI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 09 JUNI, 2015

I. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

168. MHESHIMIWA MURTAZA ALLY MANGUNGU (KILWA KASKAZINI):

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni hatua zipi za muda mfupi na mrefu zinachukuliwa na Serikali katika kukabiliana na upungufu wa watumishi wa afya Mkoani Lindi hususani Wilaya ya Kilwa.

OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):

169. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora):- Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeweka

mifumo mbalimbali ya kusimamia Maadili ya Viongozi ili kuhakikisha kwamba majukumu ya Umma yanatekelezwa kwa namna ambayo inajenga na kulinda imani ya Wananchi juu ya Serikali yao; pamoja na mienendo ya Viongozi katika utekelezaji wa majukumu ya Umma kwa Misingi ya Uwazi, uwajibikaji, uaminifu, haki, huruma na umasikini kwa kujizuia na tamaa:-

Je, ni Viongozi wangapi ambao tayari wamefikishwa Tume ya Maadili na kuhukumwa kutokana na makosa ya

- ukiukwaji wa maadili

OFISI YA RAIS, (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):

170. MHESHIMIWA LOLESIA BUKWIMBA (BUSANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa madeni ya Walimu.

**WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA
TEKNOLOJIA:**

**171. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE
(MBOZI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Eneo la Chitete ambapo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Momba linakabiliwa na ukosefu wa mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini eneo hilo litapatiwa mawasiliano ya uhakika ya simu.

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

**172. MHESHIMIWA RAJAB MBAROUK
MOHAMMED (OLE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Shirika la Afya Duniani (WHO) linathibitisha kwamba magonjwa zaidi ya 200 duniani yanaenezwa kwa njia ya matumizi ya chakaula kisicho salama; na inakadiriwa 1/3 ya wakazi wa nchi zinazoendelea wanakabiliwa na magonjwa yatokanayo na chakula kila mwaka:-

(a) Je, hali halisi ikoje kwa Tanzania;

(b) Je, hadi sasa TFDA imeshafanya kaguzi ngapi ili kugundua Viwanda vya aina gani na vingapi ambavyo ni hatarishi vya usindikaji wa vyakula.

173. MHESHIMIWA MUHAMMAD IBRAHIM SANYA (MJI MKONGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Akina mama wengi hapa nchini hutumia vipodozi ambavyo havina viwango vinavyofaa kwa matumizi ya binadamu; pamoja na jitihada za Serikali kuzuia bidhaa hizo lakini bado zinaingizwa nchini:-

Je, ni lini Serikali itakuwa makini katika kuzuia bidhaa hizo zisiendeele kuingizwa nchini.

WIZARA YA UJENZI:

174. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi kwa kipande kilichobaki.

**175. MHESHIMIWA DIANA MKUMBO CHILOLO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-
Mhe. Rais aliahidi kujenga barabara kutoka
Singida Mjini hadi Ilongero kwa kiwango cha
Lami; na kwenye mpango wa utekelezaji wa
miaka mitano ujenzi huu ulikuwa ufanyike
katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 lakini hadi
sasa hakuna dalili ya kujenga barabara hii kwa
kiwango cha lami:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

WIZARA YA KAZI NA AJIRA:

**176. MHESHIMIWA BETTY ELIEZER
MACHANGU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na
Ajira:- Serikali imekuwa ikisema mara kwa
mara kwamba vijana wanaosoma katika Vyuo
vya Elimu ya Juu wajiandae kujiajiri baada ya
masomo yao:-

Je, Serikali inaweza kuuzeza Umma wa
Watanzania kuwa ni kwa namna gani kijana
huyu anayetoka chuoni baada ya kumaliza
masomo yake anaweza kujiajiri bila mtaji, hasa
ikizingatiwa kuwa Serikali imeshindwa hata
kumsaidia mtanzania wa kipato cha chini
kukopa kwenye benki kwa sababu ya riba
kubwa ya kati ya asilimia 18 hadi asilimia 24.

WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

**177. MHESHIMIWA DKT. HENRY DAFFA
SHEKIFU (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Kilimo cha Mazao kwa kutumia utaalam wa GMO kimeshika kasi katika Nchi za Afrika hasa Afrika Kusini, Burkina Faso nk:-

- (a) Je, Tanzania ina mpango gani wa kuanzisha kilimo hicho kinachoonyesha kuongeza uzalishaji mara dufu katika Mazao ya Pamba nk;
- (b) Je, wataalam wetu wamejifunza utaalam huo na wanatoa ushauri gani kwa aina hii ya kilimo.

**DODOMA
09 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**